# SURA YA PILI

# ANGUKO LA LUSIFA(FALL OF LUCIFER)

## *Lusifa(Lucifer) ni nani?*

Jina lusifa limetumika kwenye New King James(NKJV) na pia kwenye "Bible With Strong Concordance" ambapo kwenye biblia yetu ya Kiswahili imetasafriwa kama nyota ya alfajiri/au mwana wa asubuhi "morning star".Pia Jina Lusifa hutafsiriwa kwa kiingireza kama mleta nuru"Light Bringing.Jina "**LUCIFER"**Inatokana na maneno mawili yaani "***Luc-Light mwanga/nuru na "-fer" ambayo ni "bearing" mtunza nuru au mbeba nuru***.Huko mbele tutaona hata huyu Lusifa aliumbwa kwa madini mbali mbali kama dhahabu,almasi,zumaridi,samawi,n.k yenye mng'ao wa pekee hivyo yeye hakuwa nuru halisi bali alikuwa akiakisi nuru halisi ambaye ni Kristo Yesu na Mungu Baba kwani kama tujuavyo kazi ya madini kama almasi na dhahabu ni kuakisi miale ya mwanga/nuru.

Lusifa yeye yupo kwenye kundi la Malaika waitwao Makerubi hawa wanakazi ya kulinda utukufu wa Mungu na pia kuubeba Utukufu wa Mungu(God Glory) .Ndio maana utaona hata wanaolinda njia ya kuelekea mti wa uzima ni Makerubi baada ya mwanadamu kuasi.Maana Mungu aliamua kuilinda njia ya kuelekea mti wa uzima maana mti wa uzima ulikuwa ukimwakilisha Yesu baada ya mwanadamu kuasi kama angekula tunda la uzima asingeweza kuokolewa angekuwa mwanadamu mtenda dhambi asiyeweza kusamehewa kama walivyo Malaika walioasi wao hawawezi kusamehewa maana hawana nafsi kama sisi hivyo hawawezi kuokolewa na kuokoka na Yesu hakufa msalabani kwa ajili yao.

Bwana Mungu akawafanyia Adamu na mkewe mavazi ya ngozi, akawavika.

**Mwanz.3:22-24** " ***Bwana Mungu akasema, Basi, huyu mtu amekuwa kama mmoja wetu, kwa kujua mema na mabaya; na sasa asije akanyosha mkono wake akatwaa matunda ya mti wa uzima, akala, akaishi milele;kwa hiyo Bwana Mungu akamtoa katika bustani ya Edeni, ailime ardhi ambayo katika hiyo alitwaliwa.Basi akamfukuza huyo mtu, akaweka Makerubi, upande wa mashariki wa bustani ya Edeni, na upanga wa moto uliogeuka huko na huko, kuilinda njia ya mti wa uzima"***

Ukisoma hapa utaona jinsi Lusifa alivyoumbwa kwenye;

***Ezek.28:13"Ulikuwa ndani ya Adeni, bustani ya Mungu; kila jiwe la thamani lilikuwa kifuniko chako, akiki, na yakuti manjano, na almasi, na zabarajadi, na shohamu, na yaspi, na yakuti samawi, na zumaridi, na baharamani, na dhahabu; kazi ya matari yako na filimbi zako ilikuwa ndani yako; katika siku ya kuumbwa kwako zilitengenezwa tayari"***

**Yoh.1:9"*Kulikuwako Nuru halisi, amtiaye nuru kila mtu, akija katika ulimwengu*"**

Hii inatupa uelewa hata sisi tulio ndani ya Kristo tumefanyika kuwa nuru ila hii nuru yetu tuna akisi nuru kutoka kwa Mungu na Kristo Yesu.

**2Kor.3:18"*Lakini sisi sote, kwa uso usiotiwa utaji, tukiurudisha utukufu wa Bwana, kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo, toka utukufu hata utukufu, kama vile kwa utukufu utokao kwa Bwana, aliye Roho"***

Hivyo tunachopaswa kujua pia huyu Lusifa(Shetani) kwa sasa hujigeuza mara nyingine awe Malaika Nuru ila yeye na watumishi wake ni watumishi na watawala wa giza kuwa makini ndugu mpendwa ili Shetani asije kukurubuni lazima chochote unachokisikia rohoni kiendane na kweli ya neno la Mungu.

**2Kor.11:14-15"*Wala si ajabu. Maana Shetani mwenyewe hujigeuza awe mfano wa malaika wa nuru.Basi si neno kubwa watumishi wake nao wakijigeuza wawe mfano wa watumishi wa haki, ambao mwisho wao utakuwa sawasawa na kazi zao*"**

Habari njema ni kwamba huyo Lusifa baada ya kuasi aliipoteza hiyo nuru ndiyo maana sasa anaitwa mkuu wa Giza na anatawala ufalme wa Giza maana ndani yake hana nuru tena.

**Ezek.28:17" *Moyo wako uliinuka kwa sababu ya uzuri wako; umeiharibu hekima yako kwa sababu ya mwangaza wako; nimekutupa chini, nimekulaza mbele ya wafalme, wapate kukutazama"***

Hapa ninaomba niingie kwenye kiini cha msukumo wa Roho Mtakatifu katika kuandika hiki kitabu ambapo ni shauku ya Roho Mtakatifu kujibu maswali mengi waliyonayo watu wa Mungu haswa vijana wa kizazi kipya maswali kama vile:-

**1.Hivi kwanini haswa Mungu aliamua kumuumba Lusifa na wakati huo alijua atakuja kuwa Shetani kwa sababu Mungu anajua yote kabla hayajatokea(Since God is Omniscient All Knowing God).**

**2.Na swali linaloendana na hilo la hapo juu ambalo wengi tunajiuliza kwanini Mungu hakumzuia Lusifa kabla hajawa Shetani kwa sababu Mungu ana Nguvu zote yaani Mungu ni Omnipotent(All Powerful)?**

**3.Kama mwanadamu aliumbwa akiwa Mkamilifu(Perfect) Shetani aliwezaje kumjaribu mwanadamu hadi kumuasi Mungu?**

Labda nijibu kwa namna hii Mungu haku muumba Lusifa(Lucifer) ili aje kuwa Shetani ila ni ukengeufu wa Lusifa mwenyewe kwani aliumbwa na moyo ambao ulikengeuka kwa kutamani kuwa kama Mungu ili aabudiwe na Malaika na viumbe wengine na hiki kiburi Chake(His Pride) na Uasi wake(His Rebellion) kilimfanya atupwe duniani alipotaka kuvamia mbingu baada ya kuwashawishi theluthi moja ya Malaika walioamua kuasi naye ili wapindue utawala wa Kiti cha Enzi cha utawala cha Mungu Mwenyezi.

## Sababu za Mungu kumuumba Lusifa

Twende Pamoja tunaposoma maandiko cha kuzingatia ni kuwa kwenye biblia ni sehemu chache sana utaona biblia ikitaja Asili ya Shetani na mapepo hii inatupa kutambua kuwa Mungu amekusudia tumjue Zaidi yeye maana neno la Mungu lipo wazi linatuambia tumjue sana Mungu ndipo mema na amani vitakapotujia(**Ayub.22:21**).

Tukisoma Kitabu cha Nabii **Isaya 14:12-16** tutakutana na maneno yafuatayo;

***" Jinsi ulivyoanguka kutoka mbinguni, Ewe nyota ya alfajiri, mwana wa asubuhi! Jinsi ulivyokatwa kabisa, Ewe uliyewaangusha mataifa! Nawe ulisema moyoni mwako, Nitapanda mpaka mbinguni, Nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu; Nami nitaketi juu ya mlima wa mkutano, Katika pande za mwisho za kaskazini. Nitapaa kupita vimo vya mawingu, Nitafanana na yeye Aliye juu.***

***Lakini utashushwa mpaka kuzimu; Mpaka pande za mwisho za shimo.***

***Wao wakuonao watakukazia macho, Watakuangalia sana, wakisema, Je! Huyu ndiye aliyeitetemesha dunia, Huyu ndiye aliyetikisa falme***.

Tukisoma biblia ya kiingereza haswa New King James Version(NKJV) imeandikwa "***How you have Fallen from Heaven,O Lucifer,son of morning!How you are cut down to the ground,You who weakened the nations!***

Kulingana na biblia hii ya kiingereza inamtaja moja kwa moja malaika anayeitwa Lusifa akianguka kutoka mbinguni(eneo) kwa sababu kuna tofauti ya mbinguni na mbingu tutaona hizo tofauti hapo mbele na utaona kutoka hapo(mbinguni) alitupwa katika dunia hii yaani alitupwa hadi kwenye nchi na akashushwa hadi kuzimu na hapo ndipo palipo makao ya huyu malaika Lusifa aliyekuja kuitwa Shetani/Ibilisi ambaye aliasi na kuwarubuni theluthi moja ya malaika alioasi nao na wakatupwa wote.

Hili Anguko la Lusifa ndilo ambalo Yesu aliliona anasema nalimuona Shetani akianguka kama Umeme kwenye **Luk.10:18*" Akawaambia, Nilimwona Shetani, akianguka kutoka mbinguni kama umeme"***

*Ijapokuwa huu mstari unatufundisha siri nyingine ya kuwa popote injili inapohubiriwa Shetani huanguka na Ufalme wake husambaratika maana kazi ya injili ni kudhhiirisha Ufalme wa Mungu na injili ina kazi pia ya kuusimika ufalme wa Mungu duniani.*

Kulingana na kitabu cha **Ufun.12:3-4** inatuambia hivi:-

"***Ikaonekana ishara nyingine mbinguni; na tazama, joka kubwa jekundu, alikuwa na vichwa saba na pembe kumi, na juu ya vichwa vyake vilemba saba. Na mkia wake wakokota theluthi ya nyota za mbinguni,***